




(imageless edition)

- Rukia Nantale
- Benjamin Mitchley
- Matteo E. Mwita
- Kiswahili / French
- || Level 5



Simbegwire

Simbegwire



Storybooks Canada

storybookscanada.ca

Simbegwire / Simbegwire


Written by: Rukia Nantale

Illustrated by: Benjamin Mitchley

Translated by: (sw) Matteo E. Mwita, (fr) Alexandra

Danahy


This story originates from the African Storybook (africanstorybook.org) and is brought to you by Storybooks Canada in an effort to provide children's stories in Canada's many languages.



This work is licensed under a Creative Commons

[Attribution 3.0 International License.](https://creativecommons.org/licenses/by/3.0)


<https://creativecommons.org/licenses/by/3.0>



Simbegwire alihuzunika mama yake alipofariki. Baba yake alijitahidi kumtunza mwanaye. Taratibu wakaanza kuwa wenye furaha tena, bila ya Mama Simbegwire. Kila asubuhi walikaa na kupanga mipango ya siku inayofuata. Kila jioni waliandaa chakula cha jioni pamoja. Baada ya kuosha vyombo, baba yake Simbegwire alimsaidia kufanya kazi zake za shule.

...


Quand la mère de Simbegwire décéda, Simbegwire fut très triste. Son père essaya de son mieux de prendre soin de sa fille. Lentement, ils apprirent comment se sentir heureux de nouveau, sans la mère de Simbegwire. Chaque matin, ils s'assoient et discutaient de la journée à venir. Chaque soir, ils cuisinaient le souper ensemble. Après avoir lavé la vaisselle, le père de Simbegwire l'aidait avec ses devoirs.



Siku moja baba yake Simbegwire alirudi nyumbani kwa kuchelewa. "Mwanangu uko wap?" aliiita. Simbegwire alimkimbia baba yake. Alisimama ghafla baada ya kumwona baba yake akiwa ameshika mkono wa mwanamke. "Nataka ukutane na mtu muhimu, mwanangu. Huyu ni Anita," alisema huku akitabasamu.

...


Un jour, le père de Simbegwire retourna chez eux plus tard que d'habitude. « Où es-tu mon enfant ? » il demanda. Simbegwire se précipita vers son père. Elle s'arrêta en chemin quand elle vit qu'il tenait la main d'une femme. « Je veux te présenter quelqu'un de spécial, mon enfant. Voici Anita, » il dit en souriant.



“Hujambo Simbegwire? Baba yako amenisimulia mengi kuhusu wewe,” alisema Anita. Lakini hakutabasamu wala kumpa Simbegwire mkono. Baba yake Simbegwire alijaa na furaha. Aliongelea jinsi maisha yatakavyokuwa mazuri watatu hao wakiishi pamoja. “Mwanangu, ni matumaini yangu kuwa utamkubali Anita kuwa mama yako,” alisema.

...


« Bonjour Simbegwire, ton père m’a beaucoup parlé de toi, » dit Anita. Mais elle ne sourit pas et ne serra pas la main de la fille. Le père de Simbegwire était content et excité. Il dit que les trois vivraient ensemble et qu’ils auraient une bonne vie. « Mon enfant, j’espère que tu accepteras Anita comme ta mère, » il dit.



Wiki iliyofuata, Anita aliwaalika Simbegwire, binamu zake, na shangazi yake kwa ajili ya chakula. Anita akaandaa vyakula vyote ambavyo Simbegwire anavipenda, na kila mmoja akala hadi akashiba. Baada ya kula watoto wakaenda kucheza huku watu wazima wakiongea. Simbegwire akajisikia furaha na jasiri. Akaamua kuwa si muda mrefu atarejea nyumbani kuishi na baba yake na mama yake wa kambo.

...


La semaine suivante, Anita invita Simbegwire, ainsi que ses cousins et sa tante, chez elle pour un repas. Quel festin ! Anita prépara tous les plats favoris de Simbegwire et tous mangèrent jusqu’à temps qu’ils soient pleins. Ensuite, les enfants jouèrent tandis que les adultes parlaient. Simbegwire se sentait contente et courageuse. Elle décida que bientôt, très bientôt, elle retournerait chez elle pour vivre avec son père et sa belle-mère.



Maisha ya Simbegwire yakabadilika. Hakuwa na muda tena wa kukaa na baba yake asubuhi. Anita alimpa shughuli nyingi sana za ndani hadi alikuwa anachoka kiasi ya kushindwa kufanya kazi zake za shuleni jioni. Alikuwa anaenda moja kwa moja kulala baada ya chakula cha jioni. Faraja pekee aliyokuwa nayo ni blanketi lenye rangi nyingi alilopewa na mama yake. Baba yake Simbegwire hakugundua kwamba binti yake alikuwa hana furaha.

...


La vie de Simbegwire changea. Elle n'avait plus le temps de s'asseoir avec son père le matin. Anita lui donnait tellement de tâches ménagères qu'elle était trop fatiguée pour faire ses devoirs le soir. Elle allait directement se coucher après le souper. Son seul confort était la couverture colorée que sa mère lui avait faite. Le père de Simbegwire ne semblait pas remarquer que sa fille était malheureuse.



Baba yake alikuwa akimtembelea kila siku. Mwisho akaja na Anita. Akampa mkono Simbegwire. "Nisamehe, nilikosea," akalia. "Utanipa nafasi kujaribu tena?" Simbegwire alimwangukia baba yake aliyekuwa na uso wa wasiwasi. Baadaye akamwenda Anita taratibu na akamkumbatia.

...


Son père lui rendit visite à chaque jour. Finalement, il vint avec Anita. Elle tendit la main vers celle de Simbegwire. « Je suis tellement désolée, petite, j'ai eu torts, » elle cria. « Me laisseras-tu essayer de nouveau ? » Simbegwire examina son père et son regard inquiet. Puis elle fit lentement un pas en avant et mit ses bras autour d'Anita.



Baada ya miezi michache, baba yake Simbegwire aliwaambia kwamba ana mpango wa kusafiri. “Itanibidi nisafiri kikazi,” alisema. “Lakini najua hakutakuwa na tatizo.” Uso wa Simbegwire ulijawa huzuni, lakini baba yake hakugundua. Anita hakusema lolote. Hakuwa na furaha.

...


Après quelques mois, le père de Simbegwire annonça qu’il serait parti pour un certain temps. « Je dois voyager pour mon travail, » dit-il. « Mais je sais que vous allez vous occuper l’une de l’autre. » Le visage de Simbegwire s’allongea, mais son père ne remarqua pas. Anita ne dit rien. Elle n’était pas contente non plus.



Simbegwire alikuwa anacheza na binamu zake alipomwona baba yake akija kwa mbali. Aliogopa kuwa baba yake angekuwa amekasirika, na akakimbilia ndani ya nyumba ili ajifiche. Baba yake alimwendea na akamwambia, “Simbegwire umempata mama mzuri. Anayekupenda na kukuelewa. Najivunia kuwa nawe na ninakupenda.” Walikubaliana kuwa Simbegwire angeishi na shangazi yake kwa muda wote atakaotaka.

...


Simbegwire jouait avec ses cousins quand elle vit son père de loin. Elle avait peur qu’il soit peut-être fâché, alors elle se précipita à l’intérieur de la maison pour se cacher. Mais son père vint la voir et lui dit, « Simbegwire, tu t’es trouvé une mère parfaite. Une mère qui t’aime et te comprends. Je suis fier de toi et je t’aime. » Ils se mirent d’accord que Simbegwire resterais avec sa tante aussi longtemps qu’elle veuille.



Mambo yakawa mabaya kwa Simbegwire. Aliposhindwa kumaliza kazi au alipolalamika, Anita alimpiga. Wakati wa chakula cha jioni Anita alikuwa chakula kingi, na kumwachia Simbegwire makombo. Kila usiku Simbegwire alikuwa analia, huku akilikumbatia blanketi la mama yake.

...


Les choses empirèrent pour Simbegwire. Si elle ne terminait pas ses tâches, ou si elle se plaignait, Anita la frappait. Et pendant le souper, la femme mangeait la plupart de la nourriture, laissant Simbegwire avec peu de restes. Chaque nuit Simbegwire s'endormait en pleurant, embrassant la couverture de sa mère.



Baba yake Simbegwire aliporudi nyumbani, alikikuta chumba chake kikiwa tupu. "Nini kimetokea, Anita?" aliuiza kwa simanzi. Anita akaelezea kuwa Simbegwire alitoroka. "Nilitaka aniheshimu," alisema. "Labda nilikuwa mkali sana." Baba yake Simbegwire aliondoka nyumbani na akaelekea kwenye kijiti. Akaenda kwenye kijiji cha dada yake kuuliza kama amemwona Simbegwire.

...


Quando le père de Simbegwire rentra chez lui, il trouva la chambre de sa fille vide. « Qu'est-ce qui est arrivé, Anita ? » il demanda, le cœur gros. La femme expliqua que Simbegwire s'était sauvée. « Je voulais qu'elle me respecte, » dit-elle. « Mais j'ai peut-être été trop sévère. » Le père de Simbegwire quitta la maison et se dirigea dans la direction du ruisseau. Il se rendit au village de sa sœur pour découvrir si elle avait vu Simbegwire.



Asubuhi moja, Simbegwire alichelewa kuamka. “Wewe mtoto mvivu,” Anita aliita kwa kelele. Akamvuta Simbegwire kutoka kitandani. Blanketi lake zuri likanasa kwenye msumari na kuchanika vipande viwili.

...


Un matin, Simbegwire se leva en retard. « Paresseuse ! » cria Anita. Elle tira Simbegwire de son lit. La couverture précieuse resta accrochée sur un clou et déchira en deux.



Shangazi yake Simbegwire akampeleka nyumbani kwake. Akampatia chakula, akampeleka kitandani na akamfunika na blanketi la mama yake. Usiku ule Simbegwire akalia alipokwenda kulala. Lakini yalikuwa machozi ya furaha. Alijua shangazi yake atamtunza.

...


La tante de Simbegwire la mena chez elle. Elle donna à Simbegwire un repas chaud et la borda dans son lit avec la couverture de sa mère. Ce soir-là, Simbegwire s’endormit en pleurant. Mais ses larmes étaient des larmes de joie. Elle savait que sa tante prendrait soin d’elle.



Mama huyo akaangalia juu ya mti. Alipomwona msichana na vipande vya blanketi la rangi, akalia, "Simbegwire, mtoto wa kaka yangu!" Wakina mama wengine wakaacha kufua na wakamsaidia Simbegwire kushuka toka juu ya mti. Shangazi yake akamkumbatia na kumfariji.

...


Cette femme jeta un coup d'œil dans l'arbre. Quand elle vit la fille et les morceaux de couverture colorés, elle cria, « Simbegwire, l'enfant de mon frère ! » Les autres femmes arrêtèrent de laver et aidèrent Simbegwire à descendre de l'arbre. Sa tante l'embrassa et essaya de la reconforter.



Simbegwire alikasirika sana. Akaamua kutoroka nyumbani. Akachukua vipande vya blanketi la mama yake. Akachukua na chakula na akaondoka nyumbani. Akaiyata barabara aliyopita baba yake.

...


Simbegwire était très bouleversée. Elle décida de se sauver de chez elle. Elle prit les morceaux de couverture de sa mère, emporta de la nourriture et quitta la maison. Elle suivit le chemin que son père avait pris.



Ilipofika jioni alipanda mti mrefu karibu na kijito na akaandaa kitanda kwenye matawi ya mti. Alipokuwa analala akaimba “Maama, maama, maama, umeniacha. Umeniacha na haukurudi tena. Baba hanipendi tena. Mama unarudi lini? Uliniacha.”

...

Quand le soir arriva, elle grimpa dans un arbre près d'un ruisseau et se fit un lit dans les branches. En s'endormant, elle chanta, « Maman, maman, maman, tu m'as quitté. Tu m'as quitté et tu n'es jamais retournée. Papa ne m'aime plus. Maman, quand reviens-tu ? Tu m'as quitté. »



Asubuhi iliyofuata, Simbegwire aliimba ule wimbo tena. Wakina mama walipokuja kufua nguo zao walisikia wimbo wa huzuni kutoka kwenye mti mrefu. Wakafikiri ni upepo unatikisa matawi ya mti na wakaendelea na kazi zao. Lakini mama mmoja akasikiliza ule wimbo kwa makini.

...

Le lendemain matin, Simbegwire chanta encore la chanson. Quand les femmes arrivèrent au ruisseau pour laver leur linge, elles entendirent la chanson triste qui venait du grand arbre. Elles pensaient que c'était seulement le bruissement des feuilles et continuèrent leur travail. Mais une des femmes écouta la chanson attentivement.